Advertis

Quality, affordable and sustainable energy and water services for all




ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
www.ewura.go.tz

HabariLEO
Gwiji La Habari Tanzania

Tafuta: Tafuta

Maskani | Habari za Kitaifa | Tahariri | Makala | Wazo Langu | Michezo na Burudani | Safu | Majarida | Blog | Video | Matangazo

Ijumaa Februari 04, 2011

## Makala

# Katani kuwakomboa wakulima Kanda ya Ziwa

Imeandikwa na Clara Matimo, Mwanza; Tarehe: 25th January 2011 @ 23:59 Imesomwa na watu: 215; Jumla ya maoni: 0

ZAO la mkonge au katani lililetwa nchini na wazungu mwaka 1892.

Wazungu hao walitoka jimbo la Florida nchini Marekani. Walilileta kama zao la biashara na kukuza uchumi wa jamii.

Lakini pia wakati wanaleta mkonge, walileta mazao mengine kama vile mpira ma msufi. Mpira hutengenezwa mipira ya aina mbali mbali na msufi, hutengenezwa nguo za sufi na vifaa vingine.

Baada ya kuingiza mkonge, msufi na mpira, wazungu hao walifanya majaribio katika Bonde la Usambara mkoani Tanga, ambapo mkonge uliweza kustawi zaidi kuliko mpira na msufi.

Miaka ya 1960 na 1970, mkonge ulikuwa moja ya mazao ambayo yalifananishwa kama uti wa mgongo wa taifa, kwa kuiingizia nchi mapato kikubwa. Ulikuwa ukiingizia nchi asilimia 75 ya mapato katika soko la Ulaya.

Wakati wa ukoloni, zao la mkonge lilijiongezea umaarufu nchini na kuitwa 'dhahabu nyeupe'
yaani 'White Gold'. Umaarufu wake uliendelea hadi miaka ya 1970.

Enzi hizo, mkonge ulilimwa katika mashamba ya hekta 475,000 . Ulithaminiwa na kuendelezwa, kutokana na umaarufu wake wa kuliingizia taifa kipato kikubwa.


Umaarufu wake umekuwaukipungua mwaka hadi mwaka. Kwa wakati huu Tanzania inazalisha tani 20,000 tu, ambazo ni sawa na asilimia mbili katika mashambayenye ukubwa wa hekta 180,000.

Kiasi hicho ni kidogo sana, ikilinganishwa na kile kilichozalishwa mwaka 1964. Katika miaka ya 1960, uzalishaji wa zao hilo ulifikia tani 230,000.

Kushuka kwa uzalishaji wa katani, kumeleta athari mbali mbali katika uchumi, kama vile kupoteza ajira kwa wananchi waliokuwa wakifanya kazi katika mashamba ya mkonge. Athari nyingine ni kulikosesha taifa mapato yatokanayo na zao hilo.

Pia, baadhi ya mikoa ambako kulikuwa na wakulima wakubwa, kama Tanga na Morogoro, uchumi wake unaendelea kudorora siku hadi siku.

Bidhaa ambazo zilikuwa zikizalishwa kutokana na zao hilo, hazina soko kubwa hivi sasa; badala yake bidhaa bandia zimetapakaa karibu nchi nzima. Bidhaa hizo ni pamoja na magunia bandia, ambayo kwa sasa yanaingizwa nchini kutoka China, Thailand, Korea.



Mkonge ukiwa shambani

Habari Zaidi:

- KISWAHILI SANIFU:Usiseme kesho kesho, wenda hutaona mwisho
- Maeneo muhimu ya kihistoria Rungwe yalindwa
- Wanawake wa Parakuyo waachana na utegemezi
- Baraza la Mitihani na changamoto zake
- Kilimo Kwanza kimeinua hadhi wataalamu wa kilimo
- Serikali itenge fedha nyingi shahada za uzamili
- Changamoto ya ajali za barabarani katika jamii
- Mfumo wa Stakabadhi Ghalani wang'ara Masasi
- Wamachinga watia doa sifa ya Mwanza
- SIDO yawainua wajasiriamali mikoani
- Jinsi ya kuongeza uhitaji wa bidhaa
- Neema yaja kwa wakulima wa Kagera
- Kuwahudumia wenye VVU jukumu la wote
- Wanawake wanatatizana wenyewe
- Jinsi ya kuishi kwa furaha, amani
- Shabaha yetu iwe uongozi bora
- Tuilinde amani kwa faida ya wananchi
- Wabunge msijiume bungeni
- Mpoto mguu sawa na dawa mseto
- NYUZI BIN NYUZ:

Habari zinazosomwa zaidi:

- Balaa lingine kwa Chenge
- Salama: Jasiri aliyetangaza kuishi na virusi vya Ukimwi
- Dina Marius, mrithi wa Amina Chifupa
- 'Housigeli' anataka kuniharibia ndoa
- Vatican yamvua jimbo Askofu
- Kikwete achekecha wakuu wa wilaya
- Waliochaguliwa kujiunga kidato cha tano waongezeka kwa 22%
- Orijino Komedi, Jay Dee waitwa Iringa
- Interpol yatumika kusaka wenye zeutamu
- JK apigilia msumari wa mwisho Dowans

Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, Serikali imechukua hatua mbalimbali kufufua kilimo cha mkonge. Kutokana na juhudi hizo, hadi mwishoni mwa mwaka 2000, uzalishaji uliongezeka na kufikia tani 20,489 kutoka tani 17,340 mwaka 1997.

Kwa upande wake, Bodi ya Mkonge Tanzania nayo imejizatiti kutekeleza kaulimbiu ya serikali ya "Kilimo Kwanza" kwa vitendo, lengo likiwa ni kuinua maisha ya watanzania kwa ujumla.

Wataalamu wa Bodi ya Mkonge walifanya utafiti wa awali mwaka 2006, ulioonesha kuwa ardhi ya mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Shinyanga, Mwanza na Mara, inafaa kwa kilimo cha zao hilo.

Matokeo hayo ya utafiti huo, ndio yameifanya Bodi ya Mkongekuamua kuendeleza kilimo cha katani katika Kanda ya Ziwa, badala ya mikoa ya Kaskazini na Mashariki ya Kilimanjaro, Tanga na Morogoro tu, ambako mkonge unalimwa kwa wingi kwa miaka mingi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mkonge Tanzania, Hamis Mapinda, anabainisha sababu na malengo ya Bodi kuanzisha kilimo cha Mkonge Kanda ya Ziwa.

"Tumeona ni vyema kuanzisha zao la mkonge Kanda ya Ziwa kwa kuwa awali tulikwishafanya utafiti. Tulibaini kuwa mikoa ya kanda ya ziwa ina ardhi inayofaa kwa zao hili na pia itawasaidia wakulima kuondokana na umasikini wa kipato",
anasema.

Vilevile, anasema zao hilo halina usumbufu kama yalivyo mazao mengine, kwani ukishalilima, utaendelea kuvuna kwa miaka 10 mfululizo, kinachobakia ni kazi ya kupalilia tu.

WAZO LANGU



Watanzania tuache visingizio

SOMA | HIFADHI

SAFU



Mwenza wako anakutawala?

SOMA | HIFADHI

NYOTA WA WIKI



Mtanzania anayetikisa China

SOMA | HIFADHI

JISAJILI NASI

Jina la kwanza:

Jina la Ukoo:

Baruapepe:

TUMA



Advertis
Email: advertising
Call +255 2

Katika Mkoa wa Shinyanga, wataalamu wa kilimo, wakurugenzi na wakulima, wanaunga mkono kilimo cha mkonge, hasa baada ya kuona kilimo cha Pamba kinasuasua a kushindwa kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Anna Ngogi ni Ofisa Kilimo na Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Anasema wakazi wa Kahama wako tayari kutenga ardhi yao kwa kilimo cha mkonge, endapo Bodi ya Mkonge itawawezesha, kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na pia kuwapatia mbegu bora za mkonge.

Deogratias Ruhinda ni Ofisa Mipango na Utafiti Mwandamizi wa Bodi ya Mkonge Tanzania, ambaye alitoa ufafanuzi kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa, baada ya wananchi kuonyesha hofu, kuwa wamekuwa wakiahidiwa na bodi mambo mazuri yasiyokuwa na utekelezaji.

Akifafanua, Ruhinda anasema "Kilimo cha Mkonge Kanda ya Ziwa ni matunda ya ufadhili wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), ambayo imekubaliana na Bodi ya Mkonge kufufua zao hilo nchini.

Kwa sasa tumeanza na Kanda ya Ziwa, lengo letu ni kuhakikisha mkonge unalimwa nchi nzima". Ruhinda anawataka wakazi wa Kanda hiyo, kutokuwa na hofu, kwa kuwa bodi imedhamiria kwa dhati kufufua zao hilo na ina mikakati mbalimbali.

Anasema wakulima watakaolima zao hilo, watapewa mbegu, ushauri pamoja na mafunzo ya namna ya kulitunza. Mratibu wa Mradi huo, Hassan Kibarua ni mmoja wa wajumbe waliotembelea Kanda ya Ziwa.

Anasema kilimo cha mkonge kinawezekana kwa kubadili matumizi ya ardhi kutoka kwenye mashamba madogo hadi kuwa mashamba makubwa, kupita yale yanavyolimwa mazao mengine ya chakula na biashara.

Anataja mambo muhimu yatakayozingatiwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo, kuwa ni kila mwananchi kuwa na shamba kuanzia hekta tano, sawa na ekari 12.5. Pia, wakulima wataunda vikundi vya watu 20 na watapewa vitendea kazi.

Wakulima nao hawakusita kutoa dukuduku lao, ambapo wengi walionyesha kufurahishwa na mipango hiyo ya Bodi ya Mkonge. "Wakulima wa zao hili katika wilaya ya Kahama, watanufaika kwa kujiongezea kipato na kuinua maisha yao kiuchumi", anasema Anna Mgaiywa, ambaye ni Ofisa Kilimo na Mifugo wa Kijiji cha Muhongolo wilayani Kahama.

Mtaalam huyo wa kilimo alikuwa akitoa maoni yake, kuhusu kilimo cha mkonge. Viongozi mbalimbali Mkoani Shinyanga, akiwemo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Shinyanga, Marry Qorro, nao wanaonyesha kufurahishwa kwao.

Mkurugenzi huyo anasema hatua ya kuanzishwa kwa zao hilo katika Kanda ya Ziwa, ni ukombozi mkubwa, kutokana na mikoa hiyo kutokuwa na mazao maalumu ya biashara, ambayo yanaweza kuuzwa nchi za nje.

Pia, anasema zaohilo litawaongezea wananchi kipato na kuongeza mapato cha halmashauri katika mikoa husika.

**Jumla Maoni (0)**

**Tuma Maoni yako**

Jina la Kwanza:

Jina la mwisho:

Baruapepe:

Maoni yako:

0

Tuma Maoni

Wasiliana nasi mhariri@habarileo.co.tz, advertising@dailynews.co.tz
Simu:+255 22 2 127492 au 22 2 116074 au +255 22 2 110595 au 22 2 127493
HabariLeo © 2009 Haki zote zimehifadhiwa.
DailyNews Building, Plot 7, Samora Avenue, Box 9033, Dar es Salaam, Tanzania Copyright © 2009 DailyNews Media Group